- Toa mifano juu ya mafanikio yenye kudhihirisha kwamba Jumuia za Wafanyabiashara zimewahi kuleta mabadiliko ya Sera.

* Wajengee watu Imani kwamba inawezekana.

Utaratibu wa kufikia Utetezi – yaani Mwongozo.

Utaratibu wa kufikia Utetezi

- Raia kuunda vyama vya watu wanaoishi pamoja kuwakilisha matakwa ya Jumuia yao (Civil Society Organizations – CSOs).
- CSOs kuyaweka mambo yanayowahusu kitaalam kwa kuyaainisha mambo hayo kwa Wanachama wao na kufanya utafiti ili kukuza Msimamo wa Sera.
- CSOs kuwasiliana na wenye kutoa maamuzi kwa kutumia njia rasmi na isiyorasmi kwa mambo manne ya msingi ambayo ni:-
    - Sheria
    - Utetezi wa moja kwa moja.
    - Mahusiano na Umma.
    - Umma.

- Wenye kutoa maamuzi watoe taarifa juu ya maamuzi yao kwenye vyomba vya Habari na kuchapisha kwenye Gazeti la Serikali.
- Vyombo vya Habari vitoe taarifa kwa jamii husika katika Muundo unaowezesha mlisho nyuma (Feedback).

Nafasi za Jumuia za Wafanyabiashara katika Demokrasia.

Nafasi za Jumuia za Wafanyabiashara katika Demokrasia.

- Jumuia ya Wafanyabiashara ni aina mojawapo ya vyama vya Kiraia.
- Maafisa wa Serikali ni watu wenye shughuli nyingi. Jumuia za Kibiashara ni njia inayofaa zaidi kwa kuwasiliana na Serikali.
- Jumuia za Biashara zinahitaji rasilimali ili kuwasiliana ipasavyo na Serikali - tatizo la kunufaika – bure (Wote wanao nufaika hawana budi kuchangia).

Ushawishi wa Utetezi kama huduma.

- Kama unadhani Uanachama katika Jumuia ya Biashara ni aghali (yaani kutoa rasilimali ya kutosha ili kutengeneza chombo Mathubuti cha Utetezi) fikiria hali ya kutokuwa na Sauti imekufikisha wapi hadi sasa.

Utoaji Taarifa na Mafunzo kama Huduma.

- Kama unafikiri kwamba Elimu ni aghali basi jaribu Ujinga.

  Mifano: Pata Sheria husika, Kanuni, Kodi na kuendesha Semina.

Kazi za msingi za Jumuia za Biashara.

- Kujenga Mahusiano:-
- Na Serikali.
- Vyama vingine vya Kijamii.
- Vyombo vya Habari.
- Na Umma.

Kujenga Mahusiano na Serikali.

- Mikutano na Mazungumzo kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (Public – Private Sector Dialogue Conferences – PPD).
- PPD ni tukio kwa ajili ya kujenga Mahusiano na wala si tukio ambapo Masuala mbalimbali ya Utetezi yanaweza yakajadiliwa. PPD inabadilisha Mahusiano kati ya Sekta ya Umma na Sekta ya Binafsi kutoka kutoaminiana na kuwa ya kuheshimiana. Masuala Mahususi ya Utetezi yanashughulikiwa kwa kupitia ufuatiliaji wa Utetezi.
- Kutembelea mara kwa mara Ofisi za Serikali ili kupata habari – BRELA, RTO, MTO, nk.

Kujenga Mahusiano na vyama vingine vya Kijamii (Civil Society Organizations – SCOs).

Kujenga Umoja/Muungano:

- Kunachukua muda.
- Kunaleta faida – Sauti yenye nguvu.
- Sio mara zote linawezekana.
- Pata orodha ya Jumuia za Kibiashara na vyama vingine vya Kijamii kutoka kwa msajiri (RTA).
- Tengeneza mfumo wa Mawasiliano – habari kwa maneno, barua pepe, mtandao wa Kompyuta, kwa njia ya fax na matangazo ya Radio.

Kujenga Mahusiano na Vyombo vya habari.

Vyombo vya habari kwa kulipwa.

- Andaa chakula wakati wa kukutana nao.
- Viruhusu vyombo hivyo kuingia Ofisini kwa ajili ya Mikutano.

Kujenga Mahusiano na Umma.

- Miradi ya Jamii – kuifanya mizuri zaidi.
- Kufadhili matukio.
- Kuwapeleka kwenye Mafunzo.

Kuelewa utaratibu wa utungaji Sheria na Utengenezaji wa Bajeti.

- PACT – Kitini cha Kisheria
- ESRF – Utungaji wa Sera.
- Semina kwa Jumuia za Wananchi.
- Elimu ya Uraia.

KUPANGA MAJADILIANO KATI YA SEKTA YA UMMA NA BINAFSI (PPD).

Malengo ya Majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPD).

- Kuimarisha ushirikiano wa utendaji kazi kati ya Sekta ya Umma na ile ya Binafsi.
- Kujenga uelewa katika Sekta ya Umma na Binafsi juu ya ulazima na manufaa ya Majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Binafsi.
- Kujenga mazingira ya kuaminiana kati ya Sekta ya Umma na Binafsi.
- Kuhimiza uelewa juu ya Utetezi kama mchakato endelevu.
- Kuanzisha chombo maalum kwa ajili ya majadiliano katika maeneo husika – ambacho kitakutana angalau mara moja kwa mwaka.

Orodha ya Washiriki.

Sekta ya Umma – Maafisa muhimu wa Mkoa na Wilaya.

- Wakuu wote wa Idara Mkoani – RC, RAS, RTO, RPC, RPO, RAO, TRA, TANESCO, RMO.
- Wilaya – DC, DED, DAS, DTO, MPS, Mwenyekiti wa Halmashauri (Mji na Wilaya).
- Pia husisha Sekta ya Umma katika kuanzisha Washiriki.

Sekta Binafsi – Wadau muhimu.

- Jumuia zote za Kibiashara (BAS) Mkoani.
- Wanachama watarajiwa (Makampuni).
- Vyama vya Ushirika.
- Uwakilishi wa Sekta ndogo ndogo.
- Vyama vingine vya Kijamii – Vyama vya Wafanyabiashara.
- Taasisi muhimu vikiwemo Vyuo Vikuu na Wasomi wengine waliobobea.

Idadi ya Washiriki:

- Kiwango cha juu kiwe 50, lengo 40 – 50.
- Uwiano wa Sekta ya Umma na Binafsi uwe 50/50 au ½ hadi 2/3.

Mialiko.

- Eleza bayana malengo ya PPD.
- Kupeleka Mialiko mapema kwa wahusika.
- Peleka taarifa za kuwakumbusha waalikwa.
- Nani amemwalika nani – kutegemea mazingira ya Mkoa husika /Siasa (Umma kwa Umma, Binafsi kwa Binafsi).
- Rais wa TCCIA atapeleka barua kwa Wakuu wa Mikoa husika.
- Ikiwa imeratibiwa na Muungano wa Jumuia za Kibiashara (BAs), TCCIA ikiwa mwenyeji.
- Barua ya mwaliko iwe ya ukurasa mmoja ikiwa imeambatanishwa na ajenda za majadiliano.

Upelekaji wa Mialiko.

- Ziara binafsi kabla ya tukio – kujenga mahusiano mema.
- Ikiwezekana peleka mwenyewe.
- Tuma mialiko.
- Elezea tukio na sababu za tukio hilo.
- Onyesha wadhamini.
- Mialiko inaweza kubadirishwa – kwa kutegemea rasilimali.
- Weka bayana masharti ya kuhudhuria–kama ni kujilipia, hakuna posho, n.k.

Ajenda.

- Ufunguzi – Mgeni rasmi (RC, Mwenyekti).
- Mada – zinazohusiana na jambo litakalojadiliwa – Mifano juu ya mafanikio ikielezwa na waelezaji mahili.
- Wawasilishaji mada – kutoka Sekta ya Umma na Binafsi (mada zisizozidi 2 kutoka kwa kila mtoa mada sawa na jumla ya mada zisizozidi 4).
- Uwasilishaji uwe mfupi na wenye maelezo bayana ili kuruhusu muda wa kutosha kwa majadiliano.
- Msimamizi wa tukio – Muungano wa Vyama vya Jamuia za Kibiashara na Kamati ya Uratibu (Local Coordination Committee – LCC) atakuwa ndiye Mwenyeji wa tukio, TCCIA atapaswa kuwa ndiye msimamizi wa tukio.
- Sekretarieti ni muhimu iwepo kwa ajili ya kuweka kumbukumbu za tukio.
- Muda – Si zaidi ya saa 8, pungufu ya hapo ni bora zaidi.
- Kuchagua siku – kwa makubaliano kati ya Sekta ya Umma na Binafsi ikiwezekana, panga siku kwa kuzingatia (RCC) (uchangiaji gharama – Sekta ya Umma itachangia kuwaleta Maafisa wa Umma kwenye Makao Makuu ya Mikoa), iwe siku baada ya RCC au, ikiwezekana RCC iwe siku 2 ikiwa kati ya siku ya kwanza na ya pili.

Mikakati ya /Usajili wa Uanachama.

- Panga kusajili/ Wanachama kwenye PDD - jambo hili ni tata kwa sababu Muungano wa Jumuia za Kibiashara umeshiriki.
- Wajumbe wote wa LCC watapaswa kufikiri kuhusu mkakati huu wa Usajiri.
- Wajumbe wote wa LCC wawasilishe fomu zao za Uanachama na vipeperushi kwenye meza ya Uandikishaji wa Ushiriki.
- Vipeperushi vitoe maelezo ya kila Jumuia ya Kibiashara na namna ya kuwa Mwanachama.

Tafrija.

- Lengo – Usajiri wa Uanachama, kujenga Mahusiano.
- Uwiano ulio sawa wa uwakilishi wa Sekta ya Umma na Binafsi.
- Idadi ya Washiriki – lengo 70 –80.

Idadi ya Mikakati ya kuweka mipango.

- LCC itakutana mara mbili.
- TCCIA itakutana mara nyingi zaidi.
- Kamati – zitagawana kazi za kufanya na kutoa taarifa kwa Afisa Mtendaji wa TCCIA (Itaonyeshwa katika Mpango wa Utekelezaji).

Mahali pa Mkutano.

- Penye kufaa na kukubalika.
- Mfumo wa Vyombo vya kutangazia – ni muhimu sana.
- Chakula:- chakula cha mchana, chai wakati wa Mapumziko.

Bajeti.

- Iwe katika Muundo unaoainisha aina ya matumizi kwa kila Kipengele Upande wa kushoto katika hali ya wima na gharama za matumizi kwa kila Kipengele upande wa kulia katika hali ya ulalo.
- Kama kuna Mfadhili/Mhisani uwepo Mwongozo wa wazi.
- Jumla ya gharama hutegemea:
    - Kiwango cha uhusiano na Umma/Namna ya kujinadi.
    - Kama usafiri na Posho kwa Maafisa wa Serikali/Washiriki kutoka Sekta Binafsi kutoka nje ya Mji umejumuishwa au la (Uchangiaji wa gharama).

Mpango wa Utekelezaji.

- Muundo – wa jumla dhidi ya uliofafanuliwa (tumia Muundo unaofaa zaidi kwa LCC yako).
- Muundo wenye ufafanuzi unajumisha utaratibu wa Kamati kutoa taarifa.

Mtandao wa Vyombo vya habari.

- Ainisha Vyombo vya habari vilivyopo.
- Taarifa ya maandishi kwa Vyombo vya habari. Tumia muundo wa siku 2-3 kabla ya tukio na asubuhi ya siku ya tukio.
- Siku moja baada ya tukio – toa tamko kwa Maandishi.
- Mkutano na Vyombo vya habari – mara baada ya tukio – juu ya matokea ya Mkutano.
- Radio, TV, Waandishi wa habari – Waalikwe kwenye Mkutano – walipwe kwa kuhudhuria kwao.
- Tengeneza Mkanda wa Video peleka Mkanda na taarifa ya Maandishi ya Mkutano kwenye kituo cha TV - watairusha kwa gharama ndogo (lakini fanya utafiti kabla).
- Fanya mahojiano na Waandishi wa habari baada ya tukio.

Muungano wa Washirika.

- Anza mapema kujenga Muungano wa Washiriki ukijumuisha Wadau wote.
- Jukumu – kusaidia katika kupanga PPD na Ushiriki (inaweza pia ikasimamia LCC).
- Katika mwaliko, onesha kuwa PPD imewekwa na Muungano wa Jumuia za Kibiashara (BAs).
- Bandika orodha ya Washiriki wa Muungano kwenye tukio.
- Kili na kutambua michango yao.

Kamati ya Uratibu (LCC).

- LCC si kitu kilichoandikishwa, ni muungano wa Jumuia za Kibiashara ambazo zimeandikishwa.
- Kujihusisha kwa dhati kwa Wajumbe wa LCC.
- Kukubaliana juu ya taratibu kwa ajili ya Mahudhurio, kutekeleza maazimio na majukumu Kitaalam kwa kuzingatia muda uliopangwa.
- Kila LCC ihakikishe inaweka miongozo yake inayotawala Uendeshaji wake.
- Hamasisha Wajumbe wa LCC juu ya umuhimu wa muungano katika Swala zima la Utetezi.

Maazimio.

- Panga ni maazimio gani ungeyahitaji kutokana na tukio na uyawasilishe hayo maazimio kwenye PPD.
- Moja ya maazimio utakayokuwa umepanga iwe ni kuanzisha mjadala wenye utaratibu maalum ili kufikia muafaka.
- Utaratibu huo maalum utaitwa PPD, Mkoa/Wilaya – Baraza la biashara, Mkutano wa Kibiashara, n.k. – uchaguzi wa washiriki kwa eneo husika.
- Mkutano huo ufanyike angalau mara moja kwa mwaka.
- Ufuatiliaji ni muhimu.

Mikakati.

- Ianze PPD ya Mkoa ikijumuisha na Wilaya zote.
- Iwapo fedha zinapatikana inafaa vile vile kufanya PPD kwa kila Wilaya.
- PPD katika ngazi ya Mkoa, ikiwa na Ushiriki kutoka Wilayani ingekuwa ni hatua ya muhimu za mwanzo katika Suala zima la kuibua Utetezi kwa wakati ujao.

Ufuatiliaji wa Utetezi.

- Baada ya PPD, kampeni ya kwanza ya Utetezi inapaswa kujumuisha moja ya Suala muhimu ambalo ni kupata Uwakilishi (k.m. uwezo wa kuhudhuria, uwezo wa kushiriki katika majadiliano, lakini si kupiga kura) katika Kamati mbalimbali za Serikali za Mitaa pamoja na Halmashauri za fedha na mipango, n.k.
- Ni muhimu kupata haki ya kuwa mtazamaji (kusikiliza na si kushiriki katika majadiliano) katika Mikutano ya Baraza la Madiwani.

Hatua za Utetezi.

1. Pangilia Kampeni juu Utetezi

2. Bainisha mambo ya kufanya.

3. Panga kipaumbele.

4. Unda makundi ya majadiliano.

5. Tengeneza namna ya kufanya uenezaji – kwa kutumia vyombo/vitendo vya mahusiano

6. Ainisha nafasi za Sera katika masuala ya Utetezi.

7. Tekeleza Sera kwa kuitangaza/ na kujenga mahusiano.

8. Tekeleza kazi ya kutafuta kuungwa mkono na Umma/Wadau.

9. Fanya Utetezi wa moja kwa moja.

10. Tathmini mafanikio ya Kampeni.

11. Tambua/ shukuru Washiriki waliokuunga mkono, Wajumbe wa timu ya Utetezi, Maafisa wa Sekta ya Umma na Wadau wengine.

12. Pata/Sajili Wanachama wapya.

Ni nani anaendesha Utetezi.

- Jumuia Binafsi za Kibiashara.
  - Kwa mambo yanayowahusu Wanachama wao tu.
  - Kamati ya Utetezi kuendesha Utetezi.
- Muungano ya Jumuia za Kibiashara (Kamati ya Uratibu – (LCC)).
  - Katika mambo yanayo gusa zaidi ya Jumuia moja ya Kibiashara.
  - Kamati ya Uratibu kuendesha kazi ya Utetezi.
  - Ushirika Kiongozi kuongoza Kamati ya Uratibu (LCC).

Wajibu wa Kamati ya Uratibu (LCC).

- Kuunda Muungano wa Jumuiya za Kibiashara.
  - Anza mapema.
  - Husisha Wadau wengi kwa kadri inavyowezekana.
- Panga na tekeleza Kampeni za Utetezi.
- Kutana na kuweka uiano wa nafsi za Utendaji katika LCC na kufikia makubaliano.

Wajibu wa Ushiriki /Chama Kiongozi (kwa Suala hili ni TCCIA).

- Kuratibu Kampeni.
- Kutoa huduma za uchapaji.

Hatua za Utetezi Na. 1: Kupanga Kampeni.

- Kupanga Kampeni ya Utetezi kunahusisha kutengeneza mpango wa Utekelezaji wa hatua za Utetezi.
- Mpango wa Utetezi unajumuisha muda wa utekelezaji wa Kampeni na mgawanyo wa majukumu.
- Ni nani anapanga Kampeni.
  - Kwa Jumuia Binafsi ya Kibiashara ni Kamati ya Utetezi kwa kushirikiana na Kamati nyingine ndogo ndogo.
  - Kama Jumuia ya Kibiashara (BAs) haina Kamati ya Utetezi, inapaswa kuunda Kamati ya aina hiyo.
  - Kwa Muungano wa Kibiashara ni LCCs, (RLCC, DLCC W/ kwa msaada.

Kwa zote AC na LCC.

- Inatakiwa kupata watu wanaofaa – weka vigezo kwa kuzingatia taaluma.
- Kuwepo na Utaratibu kwa Wajumbe wa LCC kuwa wao ni sehemu ya LCC.
- Hamasisha Wajumbe wa LCC juu ya umuhimu wa Muungano/Umoja katika Suala zima la Utetezi.
- Kila DCC itajiwekea miongozo inayoongoza shughuli za kazi za DCC.
- Miongozo iwe na mambo yafuatayo:-

  - Kuweka kiwango cha chini cha Mikutano, Mahudhurio, Utekelezaji wa Maazimio, na Majukumu ya Kitaalam, kuzingatia muda, kumpa Mwenyekiti uwezo wa kutoa adhabu ikiwa ni pamoja na kufukuza.

- Mahitaji ya rasilimali ya Utetezi yanapaswa yazingatie Suala zima la bajeti ya Jumuia/Chama husika.
- Kwa hiyo muda wa kutengeneza Mpango wa Utekelezaji wa Utetezi unategemea bajeti ya Jumuia.

Hatua ya Utetezi Na. 2: Ainisha Matatizo.

- Kwa Muungano, inahitajika kueleza matatizo yanayoigusa Jamii kwa ujumla.
- Onesha mambo yanayo kwenda hadi Mkoa na Taifa.
- Hoja katika Masuala ya Kitaifa yanapaswa kupelekwa hadi kwenye Jumuia – ngazi ya Taifa.

Hatua ya Utetezi Na. 3: Kuweka Kipaumbele Matatizo (Masuala).

- Jambo moja haliwezi kuwahusu wote.
- Kufikia Muafaka.
- Mambo mengine yanaweza kufanyiwa kazi vizuri sana na Jumuia moja na wala sio Muungano.
- Mambo yanayotakiwa kufanyiwa kazi haraka yapewe Kipaumbele.
- Kwa Muungano/Umoja.

  - Ainisha mambo yanayo waunganisha/wahusu wote.
  - Ainisha Matatizo/mambo yenye kuleta madhara /matokeo makubwa kwa Jamii.

- Kwa Jumuia kubwa: Kamati za Sekta zinaibua mambo au matatizo na nafasi ya tatizo kwa kushirikiana na Kamati ya Utetezi ya Jumuia (AC).

Hatua ya Utetezi Na. 4: Unda Vikundi vya kazi.

- Ni aina gani ya Vikundi vya kazi (WGs).
- PPP (kwa Suala moja).
- Kunadi/mahusiano ya Umma/uenezaji.
- Matukio (chakula cha mchana, Mikutano ya pamoja).
- Ni nani awe kwenye Vikundi?.

- Wanachama wa Jumuia ya Kibiashara.
- Watu wenye Upeo au wenye Uelewa juu ya tatizo/kazi na wenye Uwezo.

- Wajibu wa Kikundi.

  - Kutekeleza mambo yote yahusuyo tatizo hilo au kazi hiyo katika Kikundi chao.

Hatua ya Utetezi Na. 5: Utafiti na Maandalizi ya hoja za Sera (PPP).

- Hatua.
- Kikundi kuandaa hoja ya Sera ya awali.
- Kikundi kuwakilisha hoja ya Sera ya awali kwenye Kamati ya Uratibu (LCC).
- Kamati ya Uratibu inaboresha hoja ya Sera ya awali.
- Kikundi (WG) hukusanya takwimu, maboresho na kuandaa upya hoja ya Sera.
- Kikundi huwakilisha tena hoja ya Sera kwenye Kamati ya Uratibu.
- Kamati ya Uratibu huongeza mchango wake kwenye hoja ya Sera.
- Kikundi hupokea maboresho hayo kwamba ni Mwisho, hutengeneza hoja ya Sera vizuri kwa kuikamilisha.
- Kamati ya Uratibu (LCC) inaidhinisha hoja ya Sera hiyo kabla haijaanza kugawanywa.
- Ugawaji wa hoja ya Sera unaanza.
- Mikutano ya Kamati ya Uratibu (LCC) kwa ajili ya kupitia hoja ya Sera ya awali ni ya muhimu sana, lakini mahudhurio inaweza kuwa ni tatizo.
- Weka Miongozo juu ya mahudhurio.
- Kama mtu hawezi kuhudhuria, atoe maelezo kwa maandishi.
- Hii inaweza kuhusisha mtu mmojawapo kutoka kwenye Kamati Tendaji (Jumuia Kiongozi) kumtembelea ili kupata michango yao ya mawazo.

WGs hoja ya Sera ya awali.

- Eneo la kuangalia.
- Tumia takwimu zilizopo.
- Ainisha takwimu ambazo hazifai.
- Fanya hoja ya Sera (PPP) kuwa rahisi na fupi – wenye kuvutiwa wataomba habari za kiina zaidi.

WG kukusanya takwimu (data) kutoka vyanzo mbalimbali.

- Serikalini.
- Wanachama wa Sekta Binafsi
- Vianzo vingine.

WG kukusanya takwimu (data) kutoka Ofisi za Serikali.

- Mahali gani pa kwenda inategemea jambo lenyewe husika.
- Kawaida wafikiriwa ni MTO, (MR Accountant Statistical Burean n.k.)
- Omba takwimu kwa maandishi.

- Tumia umaarufu /kufahamiana.
- Ngazi ya Afisa wa kumwona – Afisa wa ngazi ya chini anaweza kuwa msaada zaidi.
- Tumia watu wengine wanaoweza kusaidia.

WG kukusanya takwimu, maoni, michango, mwitikio juu ya hoja ya Sera ya awali kutoka kwa Wanachama.

- Wadau wa msingi kuunda Vikundi vilivyolengwa/ kusudiwa.
- Maswala ya mahojiano yawe mafupi, rahisi na yenye kueleweka.
- Kutoa – kwa mkono, kwa maelezo.
- Wape maswali wayajibu na uyakusanye.
- Au unajaza /jibu pamoja nao.
- Wana Kamati ya Uratibu (LCC) wanakwenda kwa Wanachama wao.
- Nenda kwa wale wanaoweza kuwa Wanachama wako.

WG kukusanya taarifa kutoka kwenye vyanzo vingine.

- ESRF.
- TCCIA.
- Taasisi ya Elimu.
- CTI, Jumuia za Kitaifa za Kibiashara.
- Internet.
- DAI – PESA /Wadhili.
- Makampuni.
- Vyombo vya habari.

Kamati ya Uratibu (LCC) kutoa michango kwenye hoja ya Sera.

- Maoni yaliyoandikwa au kufanya Mikutano ili kupata maoni – wengi wanakubali kuwa Mikutano inafaa zaidi.

Ugawaji/usambazaji wa hoja ya Sera (PPP).

- Nani anapatiwa:-

  - Jumuia ya Wafanyabiashara

  - Magazeti.

  - Serikali.

  - Umma.

  - Taasisi za Utafiti.

  - Wahisani /Wafadhili.

- Taasisi za Elimu.

- Na wengineo.

Ni lini kuanza kusambaza – PPP.

- Mnapokuwa na Mkutano wa pamoja (Roundtable - RT), unagawa PPP kabla, wakati wa Mkutano au baada ya Mkutano (RT)?.
- Mpe Mwenyekiti wa Mkutano (RT) sio zaidi ya siku moja kabla ya tukio.
- Au usitoe mambo yote mpaka wakati wa Mkutano, toa vidokezo tu.
- Kama hakuna Mkutano wa pamoja (RT) gawa hoja ya Sera (PPP) mara inapokuwa tayari – wape Maofisa wahusika n.k.

Yaliyomo kwenye hoja ya Sera (PPP).

- Mambo muhimu.

  - Kichwa cha habari/somo.

  - Mtazamo wa Jumla.

  - Mtazamo wetu (tunaofanya Utetezi).

  - Mtazamo wa wengine.

  - Hatua inayotakiwa kuchukuliwa.

  - Mambo yanayotarajiwa kutokea/kupatikana.

- Sehemu ya mtazamo wa jumla inapaswa ielezee jinsi PPP ilivyotayarishwa, jinsi takwimu zilivyokusanywa kutoka vyonzo mbalimbali (Serikali, Wanachama, na vinginevyo), Mikutano na Wanachama, kutembelea Ofisi za Serikali, Masoko n.k.
- Onesha kwamba umepata mawazo kutoka vyanzo vingi.
- Kusiwe na migongano.
- Epuka kutumia neno " mawazo ya Upinzani" neno maoni mengine halina migongano sana. Kumbuka Serikali inaiona Sekta Binafsi kama mshirika.
- Linganisha hali ilivyo mahali ulipo (Kijiji, Wilaya, Mkoani) na hali ya Mikoa mingine. Mfano gharama za Umeme katika Mkoa wa Iringa inaruhusu ukuaji wa Maendeleo ya Viwanda ukilinganisha na Mkoa wa Ruvuma.
- Kwa baadhi ya mambo/matatizo (mfano – Ukosefu wa barabara) Wakandarasi wa Sekta Binafsi wanaweza kutoa makadirio ya gharama – kuwahusisha kunakupa msingi wa msaada na chanzo cha ukweli wa mambo na takwimu.
- Tafuta mifano ya mafanikio kutoka maeneo mengine.

Hatua ya Utetezi Na. 6: Kuanzisha uenezaji /vitu vya kufanyia mahusiano na Jamii/Umma na panga kazi za Utetezi.

- Inategemea bajeti.
- Matukio ya mahusiano ni pamoja na:-

  - Kampeni za tukio lenyewe.

  - Mikutano ya pamoja.

- Uenezaji/vitu/vifaa katika mahusiano na uenezaji ni pamoja na :-

  - Kauli, mbiu ya Kampeni.

  - Vijitabu, mabango, vipeperushi n.k.

  - Vitu vya kubandika kwenye vyombo vya usafiri.

  - Fulana, Kofia, Viatu, Skafu.

  - Peleka Tangazo la tukio kwenye vyombo vya habari na fanya mahojiano kwa njia ya kawaida ya maandishi na njia ya Kisasa ikiwa ni pamoja na mtandao wa Kompyuta (Website).

  - Kwa njia ya Barua.

  - Kwa njia ya Vipasa Sauti.

  - Kwa njia ya nyimbo (mfano wimbo wa Umeme uliyoimbwa Mbinga).

Hatua ya Utetezi Na. 7: Kutekeleza Uenezaji/kazi ya mahusiano.
Kuanza tukio.

Mkutano wa pamoja (Roundtable).

- Mkutano wa pamoja (RT) sio tukio la lazima – Utetezi unaweza kufanywa kwa Utetezi wa moja kwa moja bila kuwa na Mkutano wa pamoja.
- Mkutano wa pamoja ni tukio la mahusiano na Umma na unafanyika kama kuna pesa na kama unachangia kitu cha maana kwenye juhudi za Utetezi.
- WG inatayarisha Mkutano wa pamoja (RT) – hasa kwa ajili ya kuwa na tukio lenye kuleta hamasa kubwa kwa Umma kuhusiana na jambo husika.
- Jumuia/Chama Kiongozi – inaandaa tukio kwa sababu wanao uwezo wa Kiutendaji.
- Muda gani? Saa 2 – saa 4.
- Ainisha Maofisa walengwa watakao hudhuria Mkutano wa pamoja.
- Sekta ya Umma: Maofisa wenye mamlaka katika kutoa maamuzi juu ya sera.
- Sekta Binafsi: Wajumbe wa Kamati ya Uratibu (LCC) na Wadau wengine na watu maarufu.

- Washiriki wangapi?. Washiriki 25 – 50.
- Uwakilishi Mkubwa kutoka Sekta Binafsi.
- Je wapinzani kutoka Sekta Binafsi waalikwe kwenye Mkutano wa pamoja (RT) (wale wote wanaoyapuuzia mapendekezo yenu)?.

Hoja zinazopinga ikiwa ni pamoja na wao ni nyingi.

- Waruhusu wajadili, wanaweza kuwa bado hawaelewi.
- Hoja za kuwajumuisha/kuwaingiza ni chache kuwa miongoni.
- Mahali pa kukutana – pa kufaa, pa kubalike, chakula kinaweza kutolewa kutegemea bajeti (uwezo).
- Kuchagua tarehe – haifai kufanya Karibu na RCC, kubalianeni kati ya Kamati ya Uratibu (LCC) na Maafisa wa Serikali.
- Ajenda – Muundo – Tazama mfano.
- Hoja za Sera (PPPs) ngapi ziwasilishwe kwenye Mkutano wa pamoja (RT)?.
- Nani anawasilisha?.

  - Mwakilishi wa Kamati ya Uratibu LCC anawasilisha hoja ya Sera (PPP).

- Inahitajika wa kuripoti kinachoendelea, Muwezeshaji au mwingine?.

Mialiko – Muundo – Ukrasa mmoja (1).

- Onesha malengo ya Mkutano RT.
- Inapaswa kuonesha kuwa RT imeandaliwa na Muungano wa Jumuia za Kibiashara na TCCIA kama mwenyeji.
- Peleka mialiko wiki moja hadi mbili kabla ya tukio.
- Peleka ujumbe wa kukumbushia kabla ya siku mbili.
- Nani ana Mwalika nani:-

  - Kwa Sekta Binafsi: Kamati ya Uratibu (LCC) ndio inayoalika.

  - Kwa Sekta ya Umma: Unahitaji kupitishia mialiko kwenye Serikali ya Mkoa kwa kufuata Utaratibu kulingana na mazoea ya mahali husika.

Peleka Mialiko.

- Tembelea kabla ya tukio – jenga mahusiano.
- Elezea tukio na sababu ya tukio.
- Tuma mialiko kwa washiriki kutoka Sekta Binafsi.
- Ikiwezekana peleka Mwenyewe mialiko kwa Maofisa muhimu wa Serikali.
- Onesha Wahisani.
- Inategemea rasilimali zilizopo.
- Weka wazi masharti ya kuhudhuria, kama ni kujilipia nauli wenyewe, hakuna posho n.k.

Uwasilishaji wa hoja ya Sera – PPP.

- Fanya majaribio ya Mkutano (RT) pamoja na Kamati ya Uratibu (LCC) nzima kupata maoni yao na urekebishe namna ya kuwasilisha hiyo hoja ya Sera – PPP.
- Ufunguzi uwe wa maneno mazuri kwa Sekta ya Umma (Serikali) na Sekta Binafsi sisitiza moyo wa Serikali kwa ajili ya mazungumzo.
- Toa maelezo yanayoeleza kwamba washiriki wasitegemee kupata majibu ya hoja zao kwenye Mkutano huo ila wategemee kubadilishana mawazo na kufungua milango zaidi ya majadiliano ya moja kwa moja na kwamba utafuatilia ili kupata majawabu ya tatizo au hoja husika.
- Usisome Karatasi ya hoja washiriki wataenda nazo nyumbani.
- Wasilisha mambo muhimu kwa mtindo wa mazungumzo.
- Usisome vichwa vya habari – endelea na sehemu inayofuata kwa kitu kingine kwa namna nyingine ya bila kusoma kichwa cha habari.
- Tumia mifano kwa mambo ya kweli na vielelezo waache wazungumze – toa mifano michache tu.
- Usirudie rudie.
- Kumbuka kuonesha matokeo mazuri ya mapendekezo yako juu ya kuongeza mapato ya Serikali au kupunguza gharama za Uendeshaji wa Serikali /kupunguza matumizi ya Serikali.
- Kama zipo sheria au taratibu ambazo hazizingatiwi au zinazingatiwa isivyo, nukuu Sheria au taratibu hizo na eleza kutokana na hizo

Maelezo ya Jumla kwa Mkutano wa pamoja.

- Uwe mfupi (saa 2-4)
- Kusiwe na migongano
- Kuwe na ajenda na usimamie hizo (zifuatwe)
- Kuwe na muwezeshaji/kiongozi anayeweza kuongoza mkutano.
- Mambo yaandikwe (Hoja ya Sera) ili kuongoza majadiliano.
- Hoja ya sera iwe fupi, yenye lengo maalum au ya wazi juu ya jinsi ya mabadiliko ya Sera yanayoweza kuwa mazuri kwa jamii na sio kwa kikundi kidogo cha wafanyabiashara.
- Serikali na wafanyabiashara wanapaswa kupewa fursa ya kukaa pamoja kwa mazungumzo.
- Huu ni mkutano wa faragha-usialike vyombo vya habari.
- Itisha mkutano na waandishi wa habari baada tu ya mkutano.
- Maamuzi hayafanywi wakati wa mkutano kwa hiyo, jamii ya kibiashara ifuatilie kwa wenye malaka ya kutoa uamuzi.
- Mkutano huu (RT) Unahitaji UFUATILIAJI bila ufuatiliaji, mkutano wa namna hii hauna maana.
- Ainisha kamati, watu binafsi kwa ajili ya kufanya ufuatiliaji.
- Ufuatiliaji unahusisha, utetezi wa moja kwa moja utetezi ngazi ya msingi/awali, kampeni kwa kutumia vyombo vya habari.

Hatua ya Utetezi Na. 8: Fanya kazi za kuungwa mkono na wadau wote ngazi ya msingi.

Hivi ni nini?

- Mikutano na wadau wengi ambao hawamo katika kamati ya uratibu LCC Kampeni.
- Barua-kampeni kwa kuwaandikia maofisa wa Serikali kwa kuandikwa na wajumbe/wanachama (sio Jumuia ya Biashara-BA inaweza kupigiwa debe).

Hatua ya Utetezi Na. 9: Fanya Utetezi wa moja kwa moja.

- Kama mkutano wa pamoja (RT) umefanyika, utetezi wa moja kwa moja ufanywe mara baada ya mkutano (RT).
- Utetezi wa moja kwa moja unahusisha mawasiliano ya moja kwa moja na wenye mamlaka ya kutoa maamuzi.
- Ainisha maafisa walengwa katika utetezi.
- Wajumbe maarufu wa kamati ya uratibu (LCC) watembelee maofisa walengwa wa serikali kwa ajili ya kuzungumzia kwa kiina mambo/hoja zilizowasilishwa kwenye mkutano wa pamoja (RT).
- Kabla ya kuwatembelea maofisa katika ofisi zao, andika barua ya kuomba kukutana nao.
- Kutana na maofisa wahusika-ofisini, katika mabaa, katika migahawa, kwenye michezo, kwenye club nk.
- Lenga kuwapata wafanyakazi wa chini, makarani wa maofisa katika kusaidia kupanga tarehe ya kukutana na maofisa wahusika.
- Pata wafanyakazi maarufu.
- Nenda Dodoma kukutana na Wabunge, Kamati nk.
- Andika barua juu ya masuala husika.

Hatua ya Utetezi Na. 10: Tathimini mafanikio ya kampeni ya utetezi.

- Ufuatiliaji ni muhimu.
- Marekebisho ya bajeti ya serikali juu ya masuala ya kodi.
- Ufuatiliaji kwa maofisa husika/Idara.
- Fuatilia kwa Wabunge wanaporudi mikoani baada ya kumaliza vikao vyao vya Bunge.
- Utaratibu wa kisheria ili kuwajulisha wajumbe kinachoendelea au matokeo ya Kampeni ya utetezi.

Hatua ya Utetezi Na. 11: Shukuru waliokuunga mkono, timu ya wajumbe ya utetezi, Maafisa wa serikali na wadau wengine.

- Andika barua.
- Toa shukrani kwa kukuunga mkono kwenye matukio ya kijamii (mfano kwenye warsha).
- Tembelea ofisi mbalimbali.
- Matangazo ya kulipwa kwenye vyombo vya habari.
- Eneza/sambaza maneno ya mafanikio kwa njia ya barua na mtandao wa Kompyuta.

- Wajumbe wa kamati ya uratibu (LCC) watoe taarifa ya mafanikio kwa wanachama wao.

Hatua ya Utetezi Na. 12: Pata Wanachama wapya.

- Mafanikio ya utetezi ni moja ya vyombo muhimu vya kutangaza Jumuia ya kibiashara (BA)
- Hata kutofanikiwa kwa utetezi kunaweza kuongeza Idadi ya wanachama kwa vile wanachama watarajiwa wanaweza wakaona umuhimu wa kutoa msaada wao wa kifedha ili kuimarisha juhudi za utetezi kwa wakati ujao.
- Vipande vya magazeti vinavyoonesha mtiririko wa mambo yalivyofanywa-vitunzwe.
- Fanya sherehe.
- Kama jambo fulani linawaathiri wanachama wengi na pia wasio wanachama, lakini wasio wanachama hawapendi kujiunga na kulipa ada za uanachama, jaribu kupata habari kutoka kwao ambazo zinaweza kukusaidia kufanya tathmini ya Uanachama. Kupungua au kuongezeka kwa kiasi gani.
- Wafanyabiashara wanaelewa "Pesa" zungumza lugha yao.

Tafsiri hii imetokana na Rejea zifuatazo

1. English – Swahili Dictionary – Printed in Norway 2000

2. Kamusi ya Kiswahili Sanifu ya mwaka 1981.

3. Kitini cha Kisheria (Mwongozo wa Jumuiya za Kiraia Tanzania sehemu ya kwanza na ya pili Pact-Tanzania).

4. Kamati maalum ya Utetezi – Rukwa.